

CHUO CHA SAYANSI ZA AFYA KOLANDOTO



Kama ilivyo kwenye mataifa mbalimbali duniani, Tanzania inapambana na ugonjwa wa Corona. Katika kutekeleza maelekezo na ushauri wa serikali wenye lengo la kupambana na ugonjwa huu, Mkuu wa Chuo amesitisha shughuli zote za taaluma kwa kipindi cha siku 30 kuanzia leo tarehe 18 Machi, 2020.

Wanafunzi wote walio likizo wanapaswa kubaki majumbani hadi watakapotaarifiwa kurudi. Wanafunzi walipo chuoni wanapaswa kuondoka chuoni mara moja na watapewa utaratibu wa kurejea chuoni.

Shughuli zote za chuo upande wa utawala zitaendelea kama kawaida wakati tukiendelea kusubiri maelekezo Zaidi toka serikalini kuhusiana na ugonjwa wa Corona.

Imetolewa na

PASCHAL SHILUKA

MKUU WA CHUO

18/03/2020